**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# UTAFITI WA MAKUNDI MANNE YA LUGHA BARANI AFRIKA

Idara ya Maendeleo ya Utamaduni imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kutunza vitu vya thamani vilivyopo ndani ya jamii za Watanzania wenye mila na desturi tofauti tofauti kulingana na maeneo maalu wanapopatikana. Tafiti hizi zinahusu sehemu kuu mbili nazo ni tafiti za lugha na sehemu Urithi wa Utamaduni ikijumuisha na makala mbalimbali yanayohusiana na Utamaduni wa Kitanzania.

## UTAFITI WA LUGHA, MILA NA DESTURI ULIOFANYIKA KATIKA ENEO LA HAYDOM WILAYA YA MBULU MKOANI ARUSHA

## 3.2 UTANGULIZI

Eneo la Haydom hupatikana Wilayani Mbulu Manyara. Eneo hili ina upekee wake kutokana na sifa ya kuwepo kwa makundi makuu manne ya lugha za kijamii; Wabantu (Wanyiramba/Wanyisanzu) Wanailo (Wadatoga); Wakhoisa (Wahadzabe) na Wakushi (Wairaqw). Inasemekana kwamba Mbulu ni eneo pekee ya Bara la Afrika ambapo makundi manne ya lugha yanapatikana sambamba na utofauti wao kihistoria, shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo ufugaji na uwindaji.

## 3.1 JAMII YA WADATOOGA

### 3.1.1 Historia

Wadatooga au Watatooga ambao hujulikana kama ***'Wabarbaig'*** au '**Wataturu**' ni jamii ya kinailotiki ya nyanda za juu ambayo hupatikana Kaskazini mwa Tanzania hasa katika Wilaya za Mbulu na Hanang Mkoani Manyara, Arusha, Singida na Mara japo katika miaka ya hivi karibuni wamesambaa nchi nzima ya Tanzania kwa ajili ya kusaka malisho ya mifugo yao. Kuna aina mbili za Wanailotiki ambazo ni Wanailotiki wa Nyanda za juu yaani ambao ni jamii za Wadatooga wa Tanzania, Dorobo na Kalenjin wa Kenya na Wanailotiki wa nyanda tambarare yaani Wamasai na Luo wa Kenya.

Kama Wanailotiki wengine, asili ya Wadatooga ni Sudan na Magharibi mwa Ethiopia na walifuata Bonde la mto Nile (ndio maana wanaitwa Nilotes) kuelekea Kusini. Wadatooga (pia huitwa Wataturu au Wamang'ati) ni kabila la watu wa Kiniloti nchini Tanzania wanaoishi hasa katika mikoa ya Manyara, Mara, Arusha na Singida. Katika Sensa ya Mwaka 2000 idadi ya wadatooga inakadiriwa kuwa 87,978.

Inasemekana kuwa jamii hiyo imegawanyika katika matabaka kumi na sita (16) ambayo ni; Buradida, Rotegen, Isimejeng, Gidang'oda, Bajut, Hojaboo, Biyamjida, Tarorajig, Bisiyeda, Logh'a, Majiojeg, Tarorajig, Bisiyoda, Nyanyaud, Utatu na Darargwajeg.

### 3. 1.2 MILA NA DESTURI

**Nyumba za asili**

Nyumba za jamii ya Datooga ni za tembe ambazo hutengenezwa kwa miti pembeni na juu huezekwa kwa miti, nyasi na udongo na kukandikwa kwa matope; na nyumba hizo hujengwa kwa mpangilio ufuatao:

**Wanaume wa Kidatooga na vijana wa kiume** huishi katika nyumba yao inayoitwa "**Hulanda**" ambayo huwa mbele ya nyumba zote kwa ajili ya ulinzi wa familia na mifugo ambapo ndani ya nyumba hiyo kitanda cha vijana wa kiume huwekwa karibu na mlango.

**Nyumba ya Mke Mkubwa na wasichana** ambapo karibu na mlango huwekwa kitanda cha wasichana ikifuatiwa na chumba cha mama kwa ndani na kufuatiwa na nyumba ya ya tatu ya mke mdogo.

### 3.1.3 Miiko

Wadatooga hawali nyama ya nguruwe (hasa **ngiri pori**) na nyama ya punda. Jamii ya Barbayiga na Gisamjanga hawaoi wala kuolewa katika jamii ya **Gidang`odiga** (Karera kama wengi wanavyofahamu) ambao ni Wadatooga wahunzi, yaani wanaotengeneza mikuki, mishale, shoka, visu, bangili nk. Japo wanashirikiana nao kibiashara na mambo mengine katika jamii.

Mwanamke aliyeolewa ni mwiko kutaja jina la baba Mkwe wake au jina linalofanana na la mkwe wake, yaani baba mkwe wake kama anaitwa Gidagehandu (**James)** haruhusiwi kusema Gidagehandu (**James**) au chochote chenye matamshi yanayolandana na Gidagehandu. Mama wa Kidatooga haruhusiwi kuoga nje ya boma.

Mwanamke wa Kidatooga haruhusiwi kutoka nje ya boma kama hajavaa **Hanang`wenda** (sketi ya ngozi anayovalishwa siku anaolewa kama ishara ya pete).
Mama wa Kidatooga na watoto wadogo hawaruhusiwi kunywa pombe ya kiasili **(Gesuda)** lengo ni kuwazuia wasilewe wasije wakashindwa kutekeleza majukumu ya kulea familia. Kijana wa kiume aliyeua au kupiga mtu haruhusiwi/mwiko kufanyiwa jando na adhabu hiyo ni mpaka kufariki kwake.

### 3.1.4 Mavazi ya Asili

**Mavazi ya kiume:** Wanaume hujifunika migorori iliyotengenezwa kwa ngozi inayoitwa "**Hangda badayda**" au **Hangda Sepsepta**, na siku hizi hufunika mashuka. Jamii ya Buradida hujifunika mashuka yenye rangi nyeusi huku barbayiga hufunika mashuka yenye rangi nyekundu zilizodariziwa kwa vifungo baada ya kupaka lokaria.

**Mavazi ya Kike:** Wanawake walioolewa wanavaa sketi ya ngozi ambayo ni ishara ya pete inayoitwa **Hanang`wenda** na kwa juu huvaa "**eghwada badayda**" huku wasichana wasioolewa wakivaa "**eghawada badayda**" tu. Viatu wanavyovaa ni vya ngozi kwa jinsia zote japo hivi sasa wanavaa viatu vya tairi na baadhi yao huvaa raba na shanga kwa ajili ya umaridadi huvaliwa shingoni na bangili za plastiki huvaliwa mikononi.

### 3.1.5 Matambiko

Tambiko hufanyika kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo; balaa la ukame, kuepusha maradhi ya familia, jamii, mifugo na kuondoa nuksi. Wanawake hutegemewa sana katika shughuli za matambiko na hufanyika milimani, nyumbani na porini.

**Tambiko la familia**: hufanyika nyumbani mara nyingi hufanyika kabla jua halijachomoza na hufanyika kama matambiko mengine. Hatua ya awali ni kuandaa pombe ya **'Gesuda'**ambayo huandaliwa kwa kuchanganya maji, asali na dawa ya mti shamba uitwao ***"Sabida"*** kwenye kibuyu na kukokwa moto pembeni kwa saa ishirini na nne. Baada ya hapo huchinjwa kondoo mweusi, au

mwenye alama nyeusi na siyo mwekundu kwa kuwa katika jamii hiyo, kitu chekundu humaanisha damu. Tambiko hilo hufanyika alfajiri na mapema kwa kunywa pombe ya kienyeji ambayo ni gesuda na kumwagamwaga kwenye zizi la ng'ombe, ndani ya nyumba, kwenye vitanda na maeneo yanayozunguka nyumba kwa ajili ya kuondoa magonjwa, mifugo, familia na huisha mara tu jua linapochomoza wakiiamini kuwa maombi yao tayari yameshapokelewa baada ya jua kuchomoza.

**Tambiko la kuombea jamii**; Kabla ya kufanya matambiko wanawake hukusanyika na kwenda maeneo ya mbali na nyumba zao na kuanza kuimba nyimbo za asili kwa ajili ya kujianda na shughuli za matambiko hayo nyimbo hizo huambatana na dhamira mbalimbali kwa ajili ya kuondoa balaa zinazokumba jamii zao kwa kuombea mifugo, familia, kulaani vitendo viovu, kuepusha magonjwa yanayoikumba jamii yao na kuomba mvua.

### 3.1.6 Ngoma za Jadi

Ngoma hizi huchezwa wakati wa matamasha, matambiko, sherehe za tohara, misiba ya wazee mashuhuri/heshima kwa ajili ya sherehe za watoto wakati mama akijifungua kusogoa wanaume wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao hususan akimtelekeza mke, asipomtunza mke wakati amejifungua. Ngoma za asili mara nyingi huambatana na maudhui ya tukio husika. Kuna ngoma za aina mbili; ngoma za vijana na wanawake. wakati ngoma hizi zikichezwa.

### 3.1.7 Shughuli za kiuchumi

Jamii ya kidatooga kiasili wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo punda na kuku. Siku hizi pia wanajihusisha na uwindaji uhunzi, uvuvi wa samaki.

### 3.1.8 Chakula

**Nyama**: Wanaume ni kundi pekee ambalo wanakula sehemu mbalimbali za mnyama nundu, ulimi, kidari na moyo wanawake wakila. Sehemu zingine kama vile utumbo, maini na figo hutumiwa na wanawake na watoto. Haya ni baadhi ya mambo waliyorithi kutoka kwa vizazi vilivyopita yaani babu na bibi zao.
**Damu**: Wadatooga hugema damu ya ng`ombe bila kumwua ng`ombe, damu hiyo hupikwa yenyewe au wakati mwingine hupikwa kwa kuchanganywa na unga kama ugali.
**Maziwa**; freshi ni chakula kikuu kwa ajili ya watoto wadogo na wanaume hunywa maziwa wakati huo wanawake na wasichana wanakunywa maziwa ya mgando.

**Ugali**: Ulaji wa ugali siyo asili ya jamii ya wadatooga kutokana na mabadilko ya Sayansi na Teknolojia na mwingiliano wa utamaduni wa jamii zingine zinazowazunguka wameanza kutumia nafaka kama chakula ila siku hizi wanapika ugali wa mahindi, mtama na ulezi.

### 3.1.9 Tabia za

Wadatoga huwa na tabia zifuatazo; kusema ukweli, wajasiri, wasiri. Ni jamii inayozingatia nidhamu ya hali ya juu kwa waliowazidi umri na hasa kwa wazee, akiagizwa hakuna kubisha wala mjadala, hutekeleza kwa haraka. Inasemekana kwamba hawapendi kuishi pamoja na wakulima na ndiyo maana Wairaqw waliweza kumiliki maeneo ambayo yalikuwa yanakaliwa na Wadatooga kwani Mwiraqw anapojenga karibu na Mdatooga, huyo mdatooga huhama eneo hilo.

Inasemekana kwamba maeneo mengi yaliyokaliwa na Wadatooga ambayo ni Katesh (**Qeatesh**), Mogitu, Gehandu, Nangwa, Mulbadaw (**Marembeda**), Gidagamowd yanakaliwa na kabila la Wairaqw kwa ajili ya kufuata jamii ya wadatooga kwa kuwa ni wafugaji hivyo kihistoria inasemekana kuwa jamii hizi mbili zilikuwa zinafuatana kutokana wairaqw kufuata ardhi yenye rutuba iliyoachwa na wadatooga baada ya kuhama na mifugo wao.

### 3.1.10 Ndoa

Jamii hii ina ndoa za aina tatu; Kutumia mshenga na kupata ridhaa ya wazazi, Kukubaliana na binti na kumtorosha bila ridhaa ya wazazi na kumteka" binti bila ridhaa yake wala wazazi. Uamuzi wa kuoa hutokea baada ya kijana kumchunguza binti kwa muda wa kutosha ikiwa ni pamoja na kujua familia anayotoka hasa kuzingatia uchapaji kazi, kutokuwa mchawi na pia utajiri wa ng`ombe kwani binti wa kidatooga hupewa zawadi za ng`ombe.

**Kijana humtuma mshenga na kupata ridhaa ya wazazi;** Kijana huweza kuongea na kukubaliana na baba wa binti au kumtuma mshenga ambaye anaweza kuwa baba wa kijana anayetaka kuoa kama hakuna undugu wowote na pia kama kijana amekithi vigezo taratibu za harusi huanza. Inasemekana kuwa binti anaweza kuchumbiwa na watu hata zaidi ya 10 na wote "hushindanishwa" na kupatikana anayefaa Wazazi hutumia muda hata wa zaidi ya mwaka 1 kuchunguza familia ya kijana anayetaka kuoa kwa ajili ya kumpata mchumba anayemfaa binti yao.

Vigezo ni pamoja na tabia za familia, kama wanang`ombe au la, anaruhusiwa kuiba ng`ombe hasa kutoka kwa makabila mengine hasa wanyiramba na wanyaturu Wadatoga huamini kuwa ni jambo la ushujaa kama mwanaume akifa akiwa katika harakati za kuiba ng`ombe au akifariki kwa ajili ya mwanamke.

**Mahari;** Mahari huweza kulipwa kwa bunda la tumbako, asali na ndama (mweusi asiye na mabaka wala mawaa). Kwa kuwa wazazi wameridhia mahari huweza kuwa tumbaku au asali au ndama mweusi kabisa asiye na madoa wala mabaka na awe hajapandwa

**Harusi;** Sherehe za harusi za kidatooga huhudhuriwa na wanawake tu hata bwana harusi hatakiwi kuwa maeneo ya karibu, na hazina gharama bali

wanawake huimba nyimbo zilizojaa mafunzo kwa bibi harusi (kama kitchen Party).

Siku ya harusi mama wa binti huwekewa mafuta ya siagi kichwani kama ishara ya heshima na ufahari na binti kwa kuwa amewapa wazazi wake heshima hupewa zawadi ya ng`ombe na wazazi wake, mama hupewa zawadi ya damu iliyokaangwa na mafuta na kupeleka nyumbani kwake.

**Kukubaliana na binti na kumtorosha bila ridhaa ya wazazi;** Kijana hukubaliana na binti na kumtorosha binti baada ya kipindi kirefu hususan baada ya kupata watoto taarifa hupelekwa kwa wazazi kuwa binti yao ameshaolewa.

**Mahari;** Mara nyingi ndoa ya namna hii huambatana na mahari nyingi kutokana utoroshaji huo bila ridhaa ya wazazi wa binti kwa kulipa ng`ombe mmoja na pia binti huyo hapewi zawadi ya ng`ombe na wazazi wake badala yake kijana alimtorosha inabidi amzawadie binti ng'ombe wengi kwa kuwa inaamika kwamba mwanaume ndiye aliyemshawishi binti huyo. Njia hii hutumiwa mara nyingi hasa pale inapopeleka posa na kuonekana kuwa uwezekano wa kuoa haupo na pale inapoonekana binti na kijana wanapendana.

**Harusi;** Katika ndoa ya aina hii inapofika siku ya harusi mama wa binti hawezi kuhudhuria harusi.

**Kumteka" binti bila ridhaa yake wala wazazi;** Njia hii hutumika baada ya njia zote mbili za hapo juu kushindikana yaani pale inapotokea wazazi wa binti kutokukubali binti yao kuolewa na kijana fulani. Kijana anayehitaji kuoa huwaandaa vijana wenzake ambao humteka binti na kumwambia wazi nia yao kuwa **"tunataka kukuoa"** na mara nyingi hutekwa jioni na safari ya kuelekea ukweni huanza.

Mara nyingi ndoa ya aina hii hutumika pale kunapokuwepo kwa utajiri mkubwa wa ng`ombe kwa upande kijana anayeoa kwani ili akukubali ni lazima utampa ng`ombe wengi pengine hata 40 na hata anapokubali anakuwa chini ya ulinzi mpaka atakapojifungua. Wazazi hupewa taarifa na kama kawaida kuna faini na ukishailipa taratibu za harusi huendelea.

katika hatua zote hizo, lazima kijana muoaji alipe ng`ombe wasiopungua watano ili huyo binti akifika nyumbani kwa wakwe zake akubali kuvaa **"Hanang`wenda"** yaani sketi ya ngozi kama ishara ya pete, aingie ndani kwa ajili ya kujiandaa kuvua **"hanang`wenda"** kwa ajili ya chakula cha usiku yaani kufanya mapenzi ikiwa ishara binti huyo kukubali kuolewa. Ng`ombe hao huwahifadhi/kuwatunza kwa ajili ya kuwarithisha watoto wake wa kiume, ikumbukwe kwamba katika jamii ya wadatooga wanaume huoa mke zaidi ya mmoja hivyo kila mwanamke huhakikisha kuwa watoto kupata urithi mkubwa. Tofauti ya umri huwa si tatizo kwa mwanaume ana umri mdogo kuliko mke na

pia kaka zake au wanarika wenzake "ratta" wanaruhusiwa kufanya tendo la ndoa na mkewe bila mume kuonesha wivu wowote.

### 3.1.11 Ngoma za Asili

Barbayiga (au Barbaig kama wanavyofahamika na wengi) yaani hupiga fimbo au wapenda fimbo kutokana na kupiga fimbo wakati wanacheza ngoma, huvaa cheni iitwayo **'Graeek'** miguuni kwa ajili ya kuchezesha wakati wa ngoma, na pia kupenda kukata fimbo kila wanapoona mti unaofaa kwa fimbo ndilo kundi kubwa kuliko yote kwa wadatooga na hivyo kupelekea watu wengi kuwaita wadatooga wote kuwa ni Wabarbayiga.

### 3.1.11 Vifaa vya asili

Mkuki kwa ajili ya ulinzi na usalama wa familia na mifigo, Upinde na mshale kwa ajili ya uwindaji, vyungu, vibuyu kwa ajili ya kuweka vyakula (vipeyu) na kuchotea maji na pembe za ngombe hutumika kama vikombe kwa ajili ya kunywea pombe na ngao iliyotengenezwa kwa kwa ngozi hutumika kwa ajili ya kujikinga na mvua, jua na kujikinga wakati wa vita ngozi iliyotengenezwa mfano wa gunia kwa ajili ya kubeba mizigo na mfuko wa kubeba watoto mgongoni, Podo kwa ajili ya kuhifadhia mishale.

### 3.1. 11 Sherehe za Asili

**Sherehe za Jando (Lokhmajega);** Hufanyika porini wakati wa kiangazi ili kidonda kiweze kupona kwa haraka mara nyingi hufanyika kwa watoto wa kiume kuanzia mwaka mmoja hadi kumi na mine (1-14) kwa makundi makundi huko hufundishwa masuala ya maadili na majukumu ya wanaume pindi wanapofikia umri wa kuoa. Sherehe hii hufanyika baada ya jando na huambatana pombe ya asili ambayo hunywewa na wazee wakati vijana wakicheza ngoma za asili kwa ajili ya kuwapongeza walifanyiwa tohara.

**Unyago na ukeketaji;** Inasemekana shughuli hizi hufanyika kwa siri sana na hufanywa na kinamama. Inasemekana kwamba ukeketaji unafanyika kwa kiwango kidogo baada Serikali kuanza kupiga vita na kukataza suala hili.

**Sherehe ya kumpongeza shujaa;** Mara nyingi sherehe hizi hufanyiwa kijana wa kiume aliyeua simba wakati akichunga ng'ombe porini na wakati akirudi nyumbani hukata tawi au mwiba wa **'mti uitwao Sabida'** huo mti wa ushujaa na laana na kuweka mbele ya mlango wa boma na kuanza kuimba ili waliopo ndani waanze kutoka na kushuhudia ushujaa wake anapofika. Baada ya ushujaa huo kijana hufanyiwa sherehe na kupewa zawadi ya ngao na mkuki na baba yake pamoja na zawadi za ng'ombe kutoka kwa baba na majirani.

### 3. 1.12 Misiba

Katika jamii ya wadatooga huzika wanawake na watoto kwa kuwalaza upande na makaburi yao huchimbwa na kufunikwa udongo, maziko yao hufanyika jioni wakati jua linapoanza kuzama.

Aidha, utofauti wa mazishi kwa mzee mwenye umri kuanzia miaka 70-100 na kuheshimika na jamii hutofautiana na marehemu wengine kwani msiba wake hufanyika kwa muda wa siku nne kwa kuchinja ng'ombe dume na kufunikwa ngozi na kufungwa kwa kamba za ngozi na kaburi lake huchimbwa kwenda chini na kuchimba chumba chake ndani ya hilo kaburi na huzikwa akiwa amekalishwa mara nyingi kaburi hilo huwa mbele ya nyumba hujengwa kwa miti na hukandikwa.

Baada ya hapo maandalizi ya sherehe ya kifo hicho hufanyika **'bung'eda'** sherehe hii huchukua muda wa miezi isiyopungua mitatu na hufanyika kwa siku sita na kaburi lake lililojengwa mithili ya tanuru na hupandwa nyasi juu na kumwagiliwa ikiashiria nywele za marehemu na ishara ya kuwa hai na kuwa pamoja nao.

### 3.1.13 Mgawanyo wa majukumu

Wanaume huenda porini kwa ajili ya uwindaji kukata fito (nguzo za miti) kwa ajili ujenzi wa nyumba na usalama wa familia na mifugo wakiwa nyumbani. Wanawake hufanya shughuli za kukandika nyumba kwa matope, kuangalia familia, huchunga ng'ombe, ndama, na kuchota maji visimani.

## Lugha ya Kidatooga

Lugha ya mawasiliano ni Kidatooga, ingawa lahaja zake zinatofautiana kutokana na wingi wa matabaka ya kijamii yaliyopo miongoni mwao. Kwa hivi sasa baadhi yao huzungumza na kujifunza lugha ya Kiswahili kutoka kwa makabila mengine wakiwemo; Wanyiramba/Wanyisanzu, Wairaqw na pia watoto wao hujifunza lugha ya Kiswahili shuleni.

Yafuatayo ni baadhi ya maneno ya kidatooga na maana zake katika lugha ya Kiswahili;

| NA. | KISWAHILI | KIDATOOGA (ASIMJEGA) | DATOOGA (TATOGA) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mbolea | Shururud | Sururda |
| 2. | Wadudu | Ququda | Diyaega |
| 3. | Pembejeo | Gisireng | Mchkweka |
| 4. | Dawa | Majod | |
| 5. | Zizi | Saymod | |
| 6. | Josho | Gurash | Darash |
| 7. | Maksi | Gulang | |
| 8. | Magonjwa | Geyongwak | Geyot |
| 9. | Ngalawa | Malambod | Malembod |
| 10. | Mpiga mbizi | Ghwalsgaydod | |
| 11. | Dagaa | Budagar | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Familia | | Qenu |
| 13. | Mtemi | fuqusta | Qect |
| 14. | Ngoma | | Quteru |
| 15. | Hadithi | gewargan | |
| 16. | Nyumba | kahar | |
| 17. | Kubanika | Gidakashiki | |
| 18. | Kuchemsha | Kidashanshang’ | |
| 19. | Kukaanga | Gekarangan | |

## B. MILA NA DESTURI ZA JAMII YA WAIRAQW

### 1.0 Historia

Jamii ya Wairaqw hujulikana na kama **‘Wakushi’** hupatikana katika Mkoa wa Manyara Wilaya za; Mbulu, Babati, Hanang na Mkoa wa Arusha Wilaya ya Karatu. Asili ya jamii hii ni huko Mesopotamia Iraq Uhamiaji wao ulianza katika karne ya 4 - 6 baada ya kuzaliwa kwa Kristo kutokana na vita vya mara kwa mara. Walipita kuvuka bahari ya Sham kwa mashua na kutua Ethiopia, waliishi hapo kwa muda na waliendelea kuhama kuelekea kusini magharibi kupitia bonde la ufa kando yaziwa Victoria.

Waliendelea kuhamahama na kufika maeneo ya Singida Iramba hadi mpakani mwa Dodoma na Iringa. Wengine walielekea kusini mwa Tanzania wakati huo kulikuwepo kwa mapambano baina ya Wahehe, Wangoni na Wazimba kutokana na mapambano hayo wakarejea kuelekea kaskazini hadi sehemu ya Kondoa mahali panapoitwa Guser Tuwalay. Waliishi hapo na kuendelea na shughuli za ufugaji na kilimo kidogo.  Wengine walielekea maeneo ya Mlima Hanang’, Gallapo (Tsea Daaw).

Wakagawanyika wengine wakaelekea, Gallapo Hawa waliitwa Wagorowa na Wairaqw walipandisha mlima Dabilhadi Guser, Gangaru ambapo walifanya maskani. Baada ya muda Kiongozi wao aiiyeitwa Haymu Now wa ukoo wa Haytipe aliwaongoza hadi Nou na walifanya rnaskani yao katika maeneo ya Mama Isara eneo lote la Mama Isara lilikuwa ni ziwa wakati ule, hivyo Haymu.

Kiongozi huyo alikuwa na mtumishi wake aiiyeitwa MOYA, kiongozi huyo alitumia uganga wake kuhamisha ziwa katika eneo la Mama Isara kwa kumwagiza mtumishi wake kurusha mshale katikati ya ziwa hilo.

Mtumishi alipofanya hivyo, ziwa lilihama pamoja naye hadi katika bonde la ufa ambalo linajulikana kwa jina la ziwa manyara kwa sasa na Kiiraqw hujulikana kama "Tlawta Moya". Baada ya ziwa kuhama kiongozi huyo aliendelea kuishi hapo na watu wake na kuendelea kutawanyika katika maeneo ya Muray, Kuta, Amoa, Kainam, Suum, Datlaa, Tsaayo Wilaya ya Mbulu. Baadaye Wairaqw wakatawanyika taratibu sehemu za Karatu, Babati na Hanang kama makao

## 1.1 Chakula cha asili

Chakula chao kikuu ni nyama ya wanyamapori na wanyama wa kufuga. Walichuna nyama kwa kutumia mawe yenye ncha kali mithili ya kisu. Mapishi yao yalitokana na moto unaopatikana kwa njia ya kupekecha mti hadi moto unatokea, chombo hicho kiliitwa **(Bui na Daha).** Baadaye waligundua mazao aina ya mtama, ulezi, uwele na mboga yao ilikuwa kunde.

Nafaka hiyo husagwa kwa kutumia jiwe la mkono na unga uliopatikana ulitumika kupikia ugali mlaini (Xwante) unaofanana na uji uliopoa. Nafaka hiyo pia hutumika kutengenezea pombe ya asili ambayo ilinyweka kama viburudisho wakati wa sherehe mbalimbali za kimila.

## 1.2 Ngoma za asili

Kuna aina mbalimbali za ngoma za asili ambazo hufanyifanyika katika nyakati mbalimbali za mwaka; Ngoma ya harusi, wakati wa mavuno, wakati wa kilimo ngoma ya mbalamwezi.

**1. Ngoma ya ndani yaani ya harusi**; Ngoma hii huchezwa siku mtoto wa kike anapoolewa au wa kiume anapooa.

**2. Ngoma ya nje ya mwaka wakati wa mavuno huitwa "Gilo";** Ngoma hii huchezwa wakati wa mavuno kama ishara ya furaha na shukrani kwa Mungu.Nyimbo ya "Mudeli" huimbwa wakati wa harusi kwa kumpongeza bwana harusi na bibi harusi, nyimbo hizi huimbwa na akina mama.

Wakati wa sherehe ya shukrani za mwaka kunakuwepo na utaratibu wa maombi yaani inaitwa **"slufay"** (shukrani) pamoja na **"Giriyda".** Giriyda ni nyimbo maalum ya kuomba mambo mazuri kama vile kuombea ndoa, watoto, mazao, mifugo Amani na Ushirikiano pamoja na kuepusha mambo mabaya kama vile magonjwa ya kuambukiza na mlipo ukame na radi. Nyimbo maarufu kwa akina

mama inaitwa **"sibeli"** ni nyimbo ya shukrani kwa mungu ambaye ni **'loa'** ambaye ni nafsi ya pili

**1.3 Mavazi**

Mavazi ya asili ya Wairaqw ni ngozi. Ngozi hizo zililainishwa vizuri na kushonwa mithili ya shuka, sketi au kanga na viatu vilivyotengenezwa na ngozi.

**Vazi la kiume;** lilikuwa moja ambalo lilifunikwa kama shuka.

**Vazi la kike;** lilikuwa sketi na shuka ndogo iliyofanana na kanga. Pia wanaume na wanawake walivaa viatu vya ngozi au vilivyotengenezwa kwa tairi.

**1.4 Shughuli za kiuchumi**

Shughuli za kiuchumi katika jamii hii ni ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na kilimo cha ulezi, uwele mtama na mahindi, Kwa sasa pia hulima ngano mbaazi na alizeti. Aidha, biashara iliyokuwa inafanyika ni kubadilishana mali au mifugo kwa vifaa au zana.

**1.5 Zana za kimila**

**Zana za kilimo;** Majembe ya asili yalitengenezwa kwa kutumia miti iliyochongwa kama mithili ya jembe **"Taqhwani",** kwa ajili ya kulimia na kushindilia udongo juu ya nyumba ya Tembe.

Jembe **('Dughsay")** ni jembe lililotengenezwa na miti migumu na ilichongwa upande mmoja mithili ya chimbuo hutumika kwa ajili ya kutindua shamba jipya. Baadaye waligundua zana zilizotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi walipata kwa jamii ya wambugwe. Zana hizo zilitumika hadi majembe ya mkono yalipopatikana kutoka kwa wataalam wa nje.

Mikuki na mishale ya asili ilitengenezwa na miti iliyochongwa mfano wa mkuki wa chuma hutumika hadi sasa. Pia walitumia mawe yenye ncha kali na baadaye waligundua zana zinazotengenezwa kwa kuturnia udongo wa mfinyanzi ambazo zilikaushwa kwa moto mkali kama tofali. Vibuyu hutumika kwa ajili ya kuchotea maji, kuweka vyakula, maziwa, na vibuyu vidogo hutumika kwa ajili ya kuhifadhi mawe ya ramli, kinu hutumika kwa ajili ya kutwanga nafaka, kucheza ngoma, fimbo kwa ajili ya wazee hutembea na nazo kwa ajili ya ulinzi, ngozi kwa ajili kutengeza nguo, viatu, kulalia na podo ya kuhifadhia mishale.

**1.6 Uhifadhi wa Nafaka**

Ghala zao za asili (kuntay) hutengenezwa kwa vinyesi vya ng'ombe na majani ya miti ya asili (hutumika kama dawa ya asili) ili mazao yasishambuliwe na wadudu na majivu mithili ya chungu kubwa kwa ajili ya kuhifadhia mazao kama vile uwele, mtama, mahindi na ngano. Teknolojia hii ya uhifadhi wa nafaka kwa kuchanganya Kinyesi cha ngombe na majani ya miti iitwayo **"girgirmo"** hutumika hadi sasa kuthibiti wadudu waharibifu wa nafaka.

**1.7 Malezi**

Jamii hii ina utaratibu wa kuadilisha jamii hususan Mtoto wa kike na wa kiume mara tu baada ya mtoto kuzaliwa, hukua na kuendelea hufundishwa maadili mema ya kuishi na jamii kwa kuzingatia mila na desturi zao.

**Mtoto wa kiume;** hufundishwa na akina baba maadili ya kuishi na jamii, mbinu za kujitegemea katika kutunza familia anapokuwa ameoa.

**Mtoto wa kike;** hufundishwa na akina mama maadili mema ya kuishi na mume na namna ya kutunza familia anapoolewa na kuzaa.

**Jando na unyago**

Jando kwa watoto au vijana wa kiume hufanyika kwa makundi familia na majirani wanaofamiana huwafanyia tohara maeneo ya porini au nyumbani. Hufanyika **'Masay'** ni kinga ya asili na mganga wa jadi ikiwa ishara ya kukinga wanaotahiriwa ili wasipatwe na magonjwa na kidonda kukauka kwa haraka.

**Ukeketaji kwa wasichana;** Wasichana hufanyiwa ukeketaji na ngariba wa jadi mwenye ujuzi wa jadi na ambaye hana laana yoyote katika jamii. Ujuzi huu wa kuwafanyia ukeketaji katika jamii hii ***dhana ya kupunguza hamu ya tendo la ndoa*** kikiwa na sehemu ya mila na desturi ya yao kwa wasichana baada ya kufanyiwa ukeketaji wasichana hao hufundishwa masuala mbalimbali ikiwemo usafi, heshima, uadilifu kufanya kazi kwa bidii pamoja na namna ya kumheshimu mume wake pindi aolewapo. Katika jamii hii shughuli hizi hufanyika ikiwa ni pamoja na taratibu walizorithi kutoka kwa babu na bibi zao

### 1.8 Elimu ya jadi

Jamii hii imeendelea kufundisha watoto wao kupitia elimu ya kiasili na kijadi hususan kwa masuala yaliyohusu jamii yao kwa mfano shughuli za kilimo, ufugaji na jamii yao kwa ujumla. Kwa asili jamii hii haikupenda kuwasomesha watoto wao wakidai kuwa wakipata elimu watapotoka au mila zao kupotea. Watoto hunyimwa fursa za kwenda shule kwa ajili ya kufanya kazi za nyumbani kama vile kuchunga mifugo hasa kwa watoto wa kiume. Kwa watoto wa kike waliwazuia kwenda shule ili waolewe na wapate mali (mahari).

### 1.9 Utawala wa kijadi

Jamii hii ina mfumo wa uongozi kuanzia ngazi ya familia, ukoo na jamii kwa ujumla na kiongozi wao anajulikana kama **"Kahamusmo"** ambaye hushughulikia masuala ya kimila ikiwemo; kwa ajili maadili, majanga kama vile ukame magonjwa na kuomba mvua, kuandaa mikutano ya hivyo yeye ni msemaji mkuu wa jamii pamoja na hayo ana jukumu la kwenda kwa Waganga wa jadi kama vile "**Manda do Bayo"** kwa ajili ya kutatua matatizo ya jamii **"Manda do Bayo"** ni wataalamu wa kuthibiti mambo mabaya yanayotokea katika jamii na kutuma chui kwa ajili ya kuwaadhibu na watalamu wengine wanajulikana kwa kila mwanajamii. Kiongozi msaidizi anaitwa **"Yaabusmo"** hutekeleza majukumu yyanayoelekezwa na **"Kahamusmo"**

## 1.10 Mahakama ya jadi

Adhabu hutolewa kwa taratibu za kimila zinazozingatia kosa alilotenda mhalifu. Masuala ya makosa kwa kuitisha kikao cha wazee/viongozi wa kimila na hujadiliwa na wazee wa jinsia tofauti yaani wanaume na wanawake na kutolewa uamuzi. Pia fursa hutolewa kwa masuala yaliyohusu kesi ya jinsia moja na kujadiliwa na wazee wa jinsia hiyo kwanza ili hatimaye adhabu itolewe na jamii nzima.

Watuhumiwa waliopatikana na makosa yaliyothibitika waliotozwa faini ya kimila iliyoitwa **"Dohho"** au waliagizwa kulipa fidia kwa mlalamikaji. Watuhumiwa waliokana mashtaka hata kama kuna ushahidi walipewa adhabu ya kutengea na jamii nzima. Pia kwa kesi ambazo hazina ushahidi mlalamikaji na mlalamikiwa waliapishwa kwa yote aliyoeleza ni sahihi na laana iliyotolewa kwa aliyesema uongo fotauti na hali halisi.

**Mfano;** Adhabu anayopewa kijana aliyesababisha mimba kabla ya kuoa wazee humtandika viboko akiwa ameninginizwa kwa kamba na kuwasha moto pande zote mpaka kuuawa. Mara nyingi msichana aliyepata mimba hushauriwa na kinamama kutokumtaja kijana aliyemsabishia mimba ili kijana huyo asiuawe.

**Mfano;** Msichana akifanya tendo la ndoa kabla kuolewa na kupata ujauzito hutengwa na kufukuzwa kutokana na **"metimani"** kwani msichana akipata mimba na kujifungua nyumbani anaweza kusababisha balaa au nuksi katika familia hiyo ikiwemo vifo vya watu na mifugo hivyo, ili kuepukana na balaa hizi msichana hupelekwa sehemu ya mbali na ndugu yake wa kiume na kunyolewa kwa wembe ikiwa ishara ya kumtambulisha kwa wapita njia hivyo hukaa huko usiku na mchana  mpaka apatikane mpita njia wa kumuoa na hakuna mahari yoyote kwa wasichana, msichana huyo anaweza kuliwa na fisi baada ya kuliwa na fisi au kuchukuliwa na mpita njia kijana aliyemsindikiza hurudi nyumbani kwa ajili ya kutoa taarifa kwamba msichana huyo amechukuliwa na mpita njia au kuliwa na fisi.

Kwa sasa jamii hii imepunguza adhabu hizi, kwa vijana wa kiume na kike imekuwa kitu cha kawaida kusababisha au kusabishiwa mimba kabla ya kuoana na kiwango cha wasichana kuolewa wakiwa bado hawajabeba mimba ni ndogo. Pia, wasichana hujifungua mtoto wa kwanza hadi wa pili bila kuolewa kutokana na kuacha mila na desturi zilizokuwa zinatumika katika kuwaadhibu wanaovunja misingi ya kimila.

## 1.11. Matambiko

Kabla ya jamii kufanya tambiko huenda kuhesabu mawe kwa waganga wa jadi ambao hujulikana kwa majina na kuelekezwa aina ya tambiko inayofaa kwa ajili ya kuomba dua kwa mungu wao yaani **"loa"** katika jamii hii tambiko ni njia pekee ya kukabiliana na matatizo mbalimbali ikiwemo magonjwa, ukame, radi, kuondoa mikosi, kuepusha maadui na hufanyika nyumbani, chini ya miti

mikubwa miliamani kwenye mikusanyiko ya watu ikiwemo mikutano na vikao vya kijamii. Hufanyika wakati wa mavuno kwa ajili ya kumshukuru mungu, wakati mvua zinapochelewa kunyesha

Mara nyingi shughuli za matambiko hufanyika kwa matunda na majani ya mimea ya asili iitwayo **Bori, Or'oonda, Tsangwalii, Hhamandu** pamoja na pombe ya kienyeji iliyotengenezwa kwa kuchanga unga wa mahindi na maji na kuvundikwa kwa siku tatu na kukaangwa kwenye moto hatimaye huchanganywa kwa pamoja mtama (**"manguray")** mtama huo huoteshwa kwa maji kwa siku mbili na kusagwa kwa jiwe na huitwa **"bimbila".**

Pombe ikishaandaliwa hatua inayofuata ni kuchinja kondoo dume mweusi au mwenye mabaka meusi hutumika kwa ajili ya kusafisha au kuondoa balaa, kwa hiyo kondoo hutumika kama sabuni ya kuosha machafuko yaliyopo kwenye jamii baada ya kuchinja kondoo. Utumbo wa kondoo hunyunyizwa ndani na nje ya nyumba na na kwenye mipaka au njia za kutokea ngozi ya kondoo hufungwafungwa kwenye miti na vitandani ikiwa na ishara ya kukinga au kupooza balaa lililopo katika familia au jamii.Tambiko hufanywa na wazee wateule wa kimila ambao katika ukoo wao hakuna laana zozote, yaani mtu asiyeua na ambaye hajavunjika.

**1.12 Nyumba za asili**

Nyumba za kimila zilikuwa za Msonge zilizojengwa kwa miti kukandikwa kwa matope na kuezekwa kwa nyasi ambamo ndani yake huishi familia na mifugo yao. Kutokana uvamizi na uchomaji wa nyumba uliotokana na jamii ya kimasai kuiba mifugo yao na kusababisha vifo vya watu jamii hiyo ilibadilisha mfumo wa ujenzi kutoka nyumba za msongo na kuanzisha nyumba za nyumba za tembe zilizojengwa kwa miti na kuezekwa kwa miti, nyasi na kuwekwa udongo kwa juu ili wakati jamii za kimasai zinapokwenda kuwaibia wasiweze kutambua uwepo wa nyumba.

Aidha, ndani ya nyumba hizo zilijengwa handaki kwa ajili ya kuficha mifugo na watu pindi wavamiwapo na wamasai wanapota kuiba ng'ombe. Nyumba hizi zimeanza kutoweka kutokana na jamii kuhamia kwenye ujenzi wa nyumba za bati.

Nyumba zao zilikuwa zinachororwa picha za mifugo na watu kwenye kuta kwa chokaa, majivu, udongo mwekundu, maua na mkaa. Kwenye nyumba ambayo kuna mabinti waliofikia umri wa kuolewa hukandika matope yenye ufanano na matiti kuashiria kuwa nyumba hiyo inawasicha wa kuoa.

**1.14 Ndoa na mahusiano**

**Ndoa ya kupeana;** Wazazi wa upande wa kijana hufanya mazungumzo na wazazi wa binti kuwa kijana wao amempenda na anataka kuoa, Baada ya

mazungumzo hayo hupeana kwa makubaliano ya kiwango cha mahari ambayo mara nyingi ni ng'ombe, kondoo dume na beberu.

**Ndoa ya kutoroshana;** Kijana wa kiume hukubaliana na binti na kumtorosha binti.

**Ndoa ya kulazimishana;** Wazazi wanaweza kumlazimisha binti yao, hata kama binti hampendi kijana.

**Ndoa za kupeana;** Familia ambazo wamefiwa na kijana wa kiume, kwahiyo wazazi hutoa ng'ombe wa mahari kwa wazazi wa binti na binti huyo anaweza kuwa mke halali wakati anapokuwa kwa wakwe huweza kuzaa na ndugu wa marehemu ingawa watoto huitwa kwa jina la marehemu. Umri wa kuoa au kuolewa ni kuanzia miaka 15-18. Jamii hii ilikuwa na mfumo wa kuoa mke zaidi ya mmoja hususan kwa tajiri wa ng'ombe.

**Harusi**
Sherehe za harusi huambatana na ngoma kwa kusherekea. Siku ya kwanza ni kuvalishana pete ambayo ni bangili iitwayo **"quturmoo"** Alfajiri ya siku ya pili ndugu wa wanandoa huanza huwatolea zawadi zinaweza kuwa ngo'mbe, mbuzi, kondoo na kuku. Hivi sasa, jamii imebadili mfumo wa ndoa na kuiga tamaduni za kigeni kwa kufanya harusi za kisasa na kuoa mke mmoja.

### 1.15 Mila zisizopaswa kuendelezwa na jamii
Kuna miiko mbalimbali inayofanyika katika jamii ikiwa ishara ya laana au nuksi.

- Jamii ilikuwa inawatupa na kuwaua watoto waliozaliwa na ulemavu wa ngozi (Albino) na walemavu wa viungo.

### 1.16 Mgawanyo wa majukumu
**Baba;** ni kichwa cha familia huangalia usalama wa familia na mifugo na masuala ya ujenzi wa nyumba pamoja na kutoa mafunzo kwa vijana ili kujiandaa kwa maisha ya ndoa na kufanya kazi kwa bidii.

**Mama;** hufanya shughuli za nyumbani, kuangalia watoto, kukandika nyumba wakati wa ujenzi na kushauri watoto wa kike kwa ajili ya kuwaandaa binti wao namna ya kuwaheshimu wakubwa na kufanya kazi kwa bidii.

## 2.0 Lugha za asili
**Lugha ya asili;** Lugha ya mawasiliano ni Kiiraqw. Jamii hujifunza lugha ya Kiswahili shuleni, wamishenari, kwa Warundi, Wanyiramba/Wanyisanzu kwenye Mashamba ya mikataba. Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi maneno yaliyotafsiriwa kutoka lugha ya kiiraqw kwenda Kiswahili.

| Na. | ENEO | Lugha ya Kiswahili | Lugha ya Kiiraqw |
|---|---|---|---|
| 1 | Eneo la kilimo | Mbolea | Khawaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kilimo | Dosla |
| | | Mbegu | Dahasing’ |
| | | Maksai | Aweer dosla |
| | | | |
| 2 | Vyakula | Ugali | Faa’ |
| | | Mboga | Nanuu |
| | | Maziwa | Uulwaa |
| | | Viazi | Kasi |
| | | Kande | Naa’mis |
| | | Kuchemsha | Daahhmis |
| | | | |
| 3. | Matunda | Ndizi | Aroo |

**Wahadzabe (Khoisan)**

Historia ya Wahadzabe

Wahadzabe ni kabila linaloishi Kaskazini mwa Tanzania kuzunguka Ziwa Eyasi, katikati ya bonde la ufa, eneo jirani na Serengeti. Takwimu zinaonesha kuwa kabila la Wahadzabe ni dogo sana na inakadiriwa kuwa na watu wasiozidi elfu moja kiidadi. Historia inaonesha kuwa asili ya Wahadzabe ni Tanzania.

**A. Mila na Desturi za Wahadzabe**

Msichana au mvulana anapofikia umri wa miaka 12 anavalishwa ushanga mwili mzima kisha wanawakutanisha kucheza. Michezo hiyo hufanywa kwa kukimbizana hapa na pale.

Kwa wanaume ili aweze kuoa lazima awe hodari wa kuwinda na awe ameua mnyama mkubwa kama samba au nyati. Endapo kijana atakuwa maarufu kwa uwindaji, mama wawili watakwenda kwa mama wa msichana na kumueleza kuwa kijana wao anataka kumuoa binti yao. Baada ya hapo, Bibi wa kijana anakuja kufuatilia majibu kutoka kwa mama wa msichana na kama amekubaliwa, kijana anatakiwa kupeleka nyama ya nyati au twiga au mnyama yoyote mwenye mafuta kwa mama wa msichana ili kuonesha kwamba ana uhodari wa kuwinda na anaweza kuitunza familia.

Baada ya hapo, sherehe ya harusi huandaliwa kwa panda zote mbili, kwa upande wa kijana na upande wa binti. Hatimaye sherehe hiyo humalizikia kwa binti na kijana huenda kuishi huko yaani kwa upande wa wazazi wa msichana.

Kwa ndoa za Kihadzabe, mwanamke ndiye mwenye amri ndani ya nyumba na nyumba hujengwa kwa upande wa familia ya mwanamke. Sifa kubwa ya mwanaume ni kuwa na uhodari katika kuwinda.

**Mgawanyo wa Majukumu**

Kazi ya baba katika familia ni kuwinda na kuleta nyama na matunda wakati kazi ya mama ni kuchimba mizizi. Mke ana uwezo wa kumfukuza kwa kuweka shoka nje ya nyumba.

**Mavazi ya Harusi**

Mvulana analembwa shangaa mwili mzima na ngozi kuzunguka kiuno. Msichana hufunikwa na ngozi mwili mzima na kupambwa na shangaa.

**Vyakula vya Asili**

Vyakula vya Asili vya Wahadzabe ni asali, nyama, matunda na mizizi. Mizizi inayochimbwa huitwa **'Igwe'**na huchimbwa na Wanawake. Wanawake pia hula nyama ya kobe. Vyombo vinavyotumiwa kwa chakula ni mabati ya kobe yanayojulikana kama **'kupeako'**. Pombe ya asili hutengenezwa kwa kuchanganya asali na mibuyu.

**Maisha ya Ndoa**

Mwanamke ndiyo mwenye amri katika ndoa za Wahadzabe kwani ikitokea mwanaume ametenda kosa kubwa, mwanamke huweza kumfukuza kwa kutupa shoka nje ya nyumba. Kwa mujibu wa jamii hii, shoka ndiyo nyumba yenyewe.

Moto huwashwa kwa kutumia mti wa mpome na vijiti vya Miseko.

**Mavazi ya Asili**

Mavazi ya asili kwa Wahadzabe ni ngozi za wanyama kama vile nyani, na shangaa. Aidha, viatu vyao hutengenezwa kwa ngozi. Pia, ngozi hutumika kwa kwa malazi.

**Matibabu ya Asili**

Mtu akiugua, huombewa na wazee na kwa imani anapona kabisa. Aidha, hupewa dawa aina ya mozoyo.

**Ngoma za Asili**

Ngoma huchezwa kwenye matukio ya kijamii ikiwemo harusi na kusimika viongozi wa kijadi. Aidha, kuna ngoma ambazo huchezwa na wanawake tu na zingine huchezwa na wanaume tu.

Ngoma ya wanaume tu huchezwa kwenye mlima na mnyama huchinjwa na kutolewa vitu vyote vya ndani. Ngozi ya mnyama huyo hupewa kijana alalie kwa mwezi mzima ilikiwa ni ishara ya kumtawaza kuwa kiongozi wa jadi. Aina ya wanyama ambao huchinjwa ni pofu, swala au ngili. Pia, ngoma huchezwa nyakati za usiku kwa usiri mkubwa.

Kwa kipindi cha mwezi mzima, kijana hupewa mafunzo ya mila, desturi, miiko na taratibu za jamii. Endapo kijana atatoa siri ya tukio hili, adhabu yake ni kifo.

**Matambiko**

Matambiko hufanywa kwa sababu mbalimbali mfano, mtu akila nyama ikamsababishia kuugua hadi kufa, ataombewa dua yaani atafanyiwas matambiko kwa kuua mnyama huyohuyo hadi anapona.

**Vifaa vya Asili**

Mavazi yanatengeneza kwa Ngozi hususani ya chuo, shoka, upinde na mshale kwa ajili ya kuwindia wanyama, magamba ya kobe kwa ajili ya kuwekea chakula, ushanga kwa ajili ya kuvaa mikononi na miguuni, vibuyu vya kutunzia na kunyea maji , na njuga.

## B. Lugha ya Kihadzabe

Wahadzabe ni kabila au jamii yenye watu wachche sana na hutumia lugha ya Kihadzabe kuwasiliana katika shughuli za kila siku. Wahadzabe wamezungukwa na makabila mengine kama vile Wasukuma na Wadatooga. Lugha ya kihadzabe, huzungumzwa kwa kiasi kidogo na watu wa makabila mengine yanayopatikana katika eneo hili.

Wahadzabe wana uwezo wa kuzungumza na kusikia lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ilianza kupata mashiko kwenye jamii ya wahadzabe baada ya Serikali kuanzisha shule katika maeneo yao. Vijana walianza kujifunza na kutumia lugha ya kswahili kuwasiliana.

Hapo awali, wahadzabe waliweza kuwasiliana na makabila mengine yanayowazunguka kwa kutumia ishara. Kwa hivi sasa, wanatumia lugha ya Kiswahili pale wanapowasilisiliana na jamii makabila mengine.

Wahadzabe walieleza kuwa changamoto kubwa wanayokutana nayo katika kujifunza lugha ya Kiswahili ni matamshi. Matamshi ya lugha ya Kiswahili ni magumu kuliko matamshi ya lugha ya Kihadzabe.

Kwa kuwa shughuli kuu za kila siku kwa Wahadzabe ni kuwinda, kuchima mizizi na kulina asali na kuokota matunda, msamiati mwingi umejikita kwenye maeneo hayo. Yafutayo ni baadhi ya msamiati/ maneno kwa lugha ya kihadzabe na Kiswahili kulingana na aina ya eneo au uwanja wa msamiati huo.

| Na. | Eneo/uwanja | Kihadzabe | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | Mwili wa Binadamu | Ahabee | Meno |
| | | Ukwebii | Mikono |
| | | Hatchapichiko | Sikio |
| | | Tlimako | Kichwa |
| | | Hatlebee | Nywele |
| | | Akisako | Jicho |
| | | lougogobee | Kiuno |
| | | Tutulusako | kisigino |
| | | Intawe | pua |
| | | Guliuguliko | Goti |
| | | Tsata’ | Ulimi |
| | | Awanikako | Mdomo |
| 2. | Mimea na Wanyama | Kinjapie | Wadudu |
| | | Semenegwae | Mimea |
| | | Galiandapie | Pembejeo |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| 3. | Maeneo Mchanganyiko | Henzaaha | Familia |
| | | Henzang’oo | Nyumba |
| | | Nt’ustha | Mtemi |
| | | Tzakatzaheyako | Ngoma |
| | | Nganoako | Hadithi |
| | | Bululeya | Magonjwa |
| | | Nzindi | Dawa |
| | | | |

**WABANTU (Wanyiramba/Wanyisanzu)**

**Historia ya Wabantu**

Wabantu ni watu wa asili ya Afrika Magharibi waliosambaa kwenye mikoa ya mwanza, Dodoma, Tabora na Kigoma.   Maeneo mengi ya kibantu, hutamkwa kwenye '**ba**'ikimaanisha watu.

## A. Mila na Desturi za Wabantu

### Ndoa za Asili za Kibantu

Wabantu wana Utamaduni wa kuoa mwanamke mmoja tu na baada ya kuoa na hukaa kwa mzazi wa binti kwa muda usiopungua miaka miwili mpaka motto azaliwe. Kijana akitaka kuoa, anatoa taarifa kwa Baba na Mama yake ili waweze kuamua ni familia gani inafaa kwa motto wao kupata mwenza. Familia itakayotajwa ikikubali, mshenga hutumwa na mahali kwa wazazi wa binti ambazo ni kondoo wa kike na wakiume, yaani mkaja na kilemba. Kukumilika kwa zoezi hilo hufungua njia kwa sherehe ya Harusi kufanyika.

### Masuala ya jando na Unyago

Vijana wanapofikia umri wa 10-15 yaani wakati wa kubarehe hupekekwa kwenye mafunzo ya jadi yanayojuliakana kama jando na unyago kwa muda wa mwezi mmoja. Wakiwa huko hufundishwa mambo mbalimbali ya kijamii ikiwemo, kufanya kazi, kuheshimu wakubwa, maadili ya jamii n.k. Katika jamii hii, suala la ukeketaji hakuna na halikuwahi kukubalika.

### Matambiko

Matambiko hufanyika kwa kuchinja kondoo mweusi, ng'ombe mweusi, au mbuzi mweupe aliyezaliwa usiku. Lengo la matambiko ni kuondoa matatizo yanayoikabili jamii au majanga kama vile magonjwa. Baada ya kuchinja, maombi au dua hufanywa na yule mwenye matatizo kama ni mgonjwa hulazwa juu ya ngozi huku dua zikiendelea hadi anapona. Wakati wa Matambiko, ngoma ya matambiko huchezwa na wanawake.

Aidha, huwa kuna pombe iliyotengenezwa kwa **'mtama'** kwa ajili ya kunywewa kwenye tambiko. Matambiko hufanyika kwenye mapango makubwa au nyumbani. Wanaoombwa kwenye matambiko ni wahenga yaani mababu waliotangulia mbele ya haki. Kila mwaka ifikapo mwezi wa kumi huwa tunaenda kutoa sadaka kwa Mtemi.

### Miiko

Kwa mila za Wabantu, watoto hawaruhusiwi kula mayai, moyo, na ini. Ilielezwa kuwa ini husababisha mafuta mengi mwilini na hivyo ni hatari kwa mtoto, Moyo

humafanya mtoto kuwa mwoga yaani huzalisha roho ya woga na mayai husababisha ugonjwa wa mabusha.

Mtu akizaa mapacha, ni **nuksi** (laana) kwa upande mmoja na ni Baraka kwa upande mwingine. Ni laana kwa kuwa wazazi wote wawili yaani baba na mama hutakiwa kuamka asubuhi na mapema, kukimbia uchi wa mnyama kutoka nyumbani hadi umbali fulani kung'ata mti unaojulikana kama '**mlegea'** kisha kurudi nyumbani ikiwa ni njia ya kujitakasa. Tendo la kukimbia uchi huchukuliwa kama njia ya kuwakinga mapacha na majanga kama vile radi, surua na magonjwa ya mlipuko.

Kwa upande mwingine ni baraka kwa kuwa mate ya watoto mapacha ni dawa ya kuponya sehemu ambayo umeumwa na kitu au kuumia ukitemewa mate hayo.

**Misiba ya Wabantu**

Msiba akitokea huchezwa ngoma ya 'Buntu' ikiwa ni ishara ya kumuaga marehemu kimila. Aidha, dua/tambiko hufanywa siku ya mazishi. Kwa kawaida, matanga hufanywa kwa siku tatu.

**Mgawanyo wa Majukumu**

Wanaume hufanya kazi ya kulima na kujenga nyumba kwa ajili ya familia. Wanawake hufanya kazi ya kuchunga na kuhudumia familia; watoto.

**Sherehe za Wabantu**

Kuna aina nne za sherehe/ngoma za asili za Wabantu ambazo ni:

Sherehe ya Mazao inayojulikana kwa jila la **"nkininta".** Sherehe hii hufanyika baada ya kuvuna mazao ambapo ngoma huchezwa ikiwa ni ishara ya kusherehekea mavuno yaliyopatikana.

Sherehe ya '**Buntu'**; ni sherehe ya msiba ambapo ngoma aina ya buntu hupigwa ikiwa ni ishara ya kumuaga marehemu. Sherehe hii huambatana na matambiko kwa marehemu.

Sherehe ya '**Kinyaurungu'**; sherehe hii hufanyiwa mzee wa kibantu aliyeishi miaka mingi sana au mzee sanaa anapofariki.

Sherehe ya '**Winga'**; sherehe hii ni ya harusi pale kijana na binti wanapooana huchezewa ngoma ijulikanayo kama winga.

**Vyakula vya asili vya Wabantu**

Vyakula vya asili ni pamoja na mtama, uwele, mizizi ya mitindwa, Mbuyu, matunda ya miti,viazi vitamu, mihogo na nkorongo.

**Vifaa vya Kiasili vya Wabantu**

Buntu mithili ya baragumu, Kofia za kamba za Katani, Vibuyu vya maji na chakula na kibuyu kilivhofunikwa kwa ajili ya kuhifadhi vitu nyenye ncha kali, magamba ya konokono ambayo hutumika kwa ajili ya kukwangulia sufuria, Shoka, upinde na mashale na jembe.

**B. Lugha za Wabantu**

Lugha za kibantu zina ufanano mkubwa hususani kwenye msamiati na ni kundi kubwa barani Afrika. Kwa kuzingatia makundi mawili yanayopatikana Haydom, yaani Wanyiramba na Wanyisanzu wana uhusiano wa karibu sana na huelewana na tofauti yao ipo kwenye matamshi ambapo wanyiramba hutamka kwa kuvuta maneno lakini Wanyisanzu wanatamka bila kuvuta. Maana za maneno ni sawa kwa kiasi kikubwa.

Ilielezwa kuwa Lugha za Kinyiramba na Kinyisanzu huzungumzwa kwa kiasi kikubwa na jamii zinazozunguka eneo hilo. Aidha, Wanyisanzu na Wanyiramba hutumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana na lugha za makabila mengine.

Changamoto kubwa iliyokuwa inawakabili Wabantu katika kujifunza Kiswahili ilikuwa uhaba wa shule. Lakini kwa hivi sasa wanajifunza lugha ya Kiswahili kwa urahisi kwani Serikali imeshawajengea shule kwenye maeneo yao.

Katika utafiti kuhusu msamiati wa Wanyiramba na Wanyisanzu kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kilimo, afya, ufugaji,n.k, jedwali lifuatalo litaonesha msamiati kwa lugha ya kibantu na Kiswahili.

| Na. | Eneo/Uwanja | Kinyiramba/Kinyisanzu | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | Eneo la Kilimo | Utinko | Mbolea |
| | | N’gunue | Wadudu |
| | | Matina | Mimea |
| | | Isheme | pembejeo |
| | | Mahuka | Dawa |
| 2. | Eneo la Utafiti | Lakina yani | Sampuli |
| | | Kutyatela | Nukuu |
| | | Kuyandia | Dibaji |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Pamulundo | Muhtasari |
| 3. | Eneo la Ufugaji | Mpongolo | Zizi |
| | | Nsale | Chanjo |
| | | Yongelyo | Josho |
| | | Nziku | Maksai |
| | | ulyele | Magonjwa |
| 4. | Vyombo vya Uvuvi na usafirishaji | Byini | Mtumbwi,<br>Ngalawa |
| | | Boti | Boti |
| 5. | Majina na Vyeo vya Waongozaji na watumiaji wa vyombo vya majini | Mtongeli | Nahodha |
| | | Antu.alongwele | Abiria |
| | | Msoti Mumazi | Mazamiaji |
| | | Mkoa Nsambo | Mpiga mbizi |
| 6. | Majina ya Mitego ya Uvuvi | Mgono | Dema |
| | | Nyabu | Nyavu |
| | | Kokola | Kokoro |
| | | Msipi | Mshipi |
| 7. | Aina ya Samaki Wanaovuliwa | Upulu | Furu |
| | | Mbuta | Sangara |
| | | Mbungulusi | Sato |
| | | Udagala | Dagaa |
| 8. | Njia za kuhifadhi Samaki | Kuyanika | Kubanika |
| | | Kupyupya | Kuchemsha |
| | | Kuyumia | Kukaanga |
| 9. | Maeneo mchanganyiko | Antuanumbaimue | Familia |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Numba | Nyumba |
| | | Mkulu wa Ngugu | Mtemi |
| | | Mbina | Ngoma |
| | | Kalusimu | Hadithi |

**USHIKIANO WA KIMATAIFA.**

Taifa la Tanzania kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inadumisha ushirikiano na mataifa mengine duniani katika nyanja zote ili kuweza kutambulika kimataifa. Idara ya Maendeleo ya Utamaduni iliyopo ndani ya wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, inaendeleza na kudumisha ushirikiano wa Sekta ya Utamaduni na mataifa mengine duniani kwa kushiriki katika matukio mbalimbali maalumu yahusuyo utamaduni na Lugha Adhimu ya Kiswahili. Kutokana na hayo, Idara ya Utamaduni ina Mikataba mbalimbali ya kimataifa kama ; The United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO) zinazoonyesha makubaliano ya ushirikiano na uwanachama wa sekta ya utamaduni kimataifa.